**MTIHANI WA KATI YA MUHULA WA PILI 2024**

**MUDA: SAA MOJA UNUSU**

**DARASA: KIDATO CHA NNE FASIHI**

**MAAKIZO**

1) **<u>Sehemu ya A:hadithi fupi :Mapambazuko ya machweo.</u>**

…Alipigwa kalamu kazini miaka mingi iliyopita.Shirika la reli alilohudumia tangu macheo ya maisha yake lilimtimua kazini ili kupunguza idadi ya waajiriwa.Alikwenda mahakamani kutaka arudishwe kazini lakini hata kabla kesi haijaskizwa,shirika hilo lilisambaratika kutokana na hali ngumu ya kiuchumi.Hivyo,hata marupurupu yake hakupata kulipwa!Machungu yaliyompata ni sawa na yale ya kupigiliwa msumari wa moto kwenye kidonda kibichi.Shoka likamwangukia yeye miongoni mwa wengine.Matarajio yake ya kuwa na maisha mema yakaporomoka kama jabali la barafu juani.Bintiye wa pekee aliwatoroka akiwa na umri mdogo kwenda kuolewa ughaibuni.Hakuweza kustahimili urumo katika maisha asiyokuwa ameyazoea….aliketi kuchuuza vitu vyake lakini bado alikuwa akiwazia maneno ya mkewe.Kwa nini niendelee kumstahi mtu asiye na fadhila kama yule?

a) Chambua mtindo katika kifungu hiki. (alama 6)
**Msemo/nahau:alipigwa kalamu**
**Jazanda:tangu macheo ya maisha yake kumaanisha maisha ya ujana wake.**
**Nidaa:hata marupurupu yake hakupata kulipwa!**
**Tashbihi :matarajio yake ya kuwa na maisha mema yakaporomoka kama jabali la barafu juani/machungu yaliyompata ni sawa na yale ya kupigiliwa mshumari moto kwenye kidonda kibichi.**
**Uzungumzi nafsia:kwa nini niendelee kumstahi mtu asiye na fadhila kama yule?**
**Swali balagha: kwa nini niendelee kumstahi mtu asiye na fadhila kama yule?**

b) Eleza sifa za anayerejelewa katika kifungu hiki. (alama 4)
**Anayerejelewa ni Makucha.**
**Jasiri**
**Mwenye hasira**
**Mwajibikaji**
**Mcha mungu**
**Mwenye bidii**
**Fisadi**
**Mwanafunzi atolee ufafanuzi la sivyo asituzwe.**

2) **<u>Sehemu ya B:Tamthiliya ya Bembea ya maisha.</u>**

**"Ninavaa vizuri na kujivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele."**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.(alama 4)
**Msemaji:Bunju**
**Msemewa:Neema**
**Mahali: nyumbani kwao**
**Tukio/sababu:Bunju alikuwa anamweleza Neema kwamba angetaka kumsaidia kulipia mamake bili ya hospitali lakini alikuwa hana hela.**

b) Tambua kipengele cha mtindo katika dondoo hili.(alama 2)
**Taswira:ninavaa vizuri**



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Uhuishi :kujivisha tabasamu ila ndani ni viraka na huzuni tele**.

c) Tambua sifa za msemewa kama inavyojitokeza katika dondoo hili.(alama 4)
**Msemewa ni Neema**
**Ni mwenye bidii**
**Msomi**
**Mwajibikaji**
**Mwenye heshima**
**Mwenye utu**
**Mwanafunzi afafanue sifa,asipofafanua asituzwe alama**.

**3) <u>Sehemu ya C:Fasihi simulizi</u>**

Malaika nakupenda malaika

Malaika nakupenda malaika

Nami nifanyeje?

Kijana na mali sina we!

Ningekuoa malaika

Pesa zasumbua moyo wangu

Pesa zasumbua moyo wangu

Nami nifanyeje

Kijana mwenzio

Nashindwa na mali sina wee

Ningekuoa malaika.

**<u>Maswali</u>**

a) Tambua utungo huu na udhibitishe jibu lako.(alama 2)
**Wimbo wa mapenzi-malaika nakupenda malaika**.

b) Tambua nafsi neni katika utungo huu.(alama 1)
**Mvulana –mali hana ya mahari**.

c) Eleza toni inayojitokeza katika utungo huu.(alama 1)
**Toni ya kusihi/kurai**.

d) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika utungo huu.(alama 2)
**Swali balagha:name nifanyeje?**
**Takriri:malaika nakupenda malaika**
**Nidaa :nashindwa na mali sina wee!**

e) Eleza dhima ya utungo huu.(alama 4)

**Kusifu tabia au umbo la mpenzi.hutaja tabia chanya na umbo zuri la mpenzi.**

**Kutakasa hisia za anayeimba.**

**Huburudisha anayesikiliza.**

**Hukuza ubunifu.**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Ni nyenzo ya kupitisha maarifa au elimu ya jamii**.

4) **Sehemu ya D: ushairi andishi**

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili

Vitisho kamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikosee simile, magalacha, si gurudumu mwili

Vingekuwepo viraka, kuutia, ngeushuruti mwili,
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili,
Upya ukaungulika, kuvutia, roho na wake mwili

Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili,
Sihofu kupata mawi, sitajuta, kupigania mwili,
Hata kufutwa, sikawi, nitakita, kidete nao mwili

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili.(alama 2)
**Kuonyesha kuwa kazi ni shughuli muhimu ila haiwezi kuzingatiwa zaidi ya afya.**
**Kuonyesha kuwa ipo haja ya kuipa afya kipaumbele kwa kuvikata vitisho vya wenye kazi/waajiri.**
**Kuukosoa uongozi dhalimu-kufutwa sikawi.**
**Kuzindua wafanyakazi.**

b) Fafanua mbinu nne za lugha zilizotumiwa katika shairi hili.(alama8)
**Matumizi ya sitiari/jazanda-si gurudumu mwili.**
**Uhaishaji-ugonjwa umepewa sifa za kutenda mwili kuudhili.**
**Matumizi ya nahau-viraka kuutia.**
**Urudiaji wa maneno/takriri-kila ubeti unaishia kwa neno mwili**.

c) Eleza toni ya shairi hili.(alama 2)
**Hasira-si gurudumu mwili**
**Machungu-ila wauma mwili.**
**Kulalamika-sihofu kupata mawi.**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

d) Ni nani anayezungumziwa na nafsineni katika shairi hili.(alama 1)
**Mwenyekazi/mwajiri.**

e) Eleza bahari ya shairi hili kwa kurejelewa.(alama 3)
Vipande **ukawafi**
Vina **ukara**
Kiishio **sabilia**

f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya nathari.(alama 4)
**Mimi kwa hakika ninaithamini kazi kwa akili na mwili isipokuwa siamini kwamba inafaa kuteseka kwa kila hali. Hasa ugonjwa unapohusika kutumia nguvu hakuwezi kunitisha/siwezi kuogopa kutumia nguvu kujitetea**.

**5) <u>Sehemu ya E: Riwaya ya Chozi la heri.</u>**

"…Mara ngapi umeponea tundu la sindano kunaswa na mashine za forodha?Je, isingekuwa mwajiri wako **<u>kuvilainisha viganja vya maafisa wa forodha,</u>**wewe na wenzako msingekuwa mmeozea kwenye magereza."

**<u>Maswali.</u>**

a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
**Huu ni uzungumzi nafsia wa Dick akiwa katika uwanja wa ndege. Hii ni baada ya Dick kubadilisha mawazo yake ya kufanya biashara haramu**.

b) Kwa kurejelea mifano mbalimbali eleza namna ambavyo maudhui yanayorejelewa na maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 6)
**Maudhui hayo ni ufisadi.**
**Lunga anafutwa kazi kwa kukosa kutia sahihi katika mradi wa kuleta mahindi aliyodai kuwa yalikuwa sumu.**
**watoto wa maskini hawapewi ruzuku na mikopo shuleni wanayofaidika ni watoto wa matajiri.**
**Wanapolisi wanakosa kuwajibikia kazi zao kwa sababu wanategemea hongo kutoka kwenye kauli ya Mwaliko.**
**Buda alitumia hongo kuwaziba macho askari wa forodha ili dawa zake zisafirishwe.**
**Bwana Mabavu anatumia hatimiliki bandia kuwapokonya familia ya Shamsi shamba lao.**
**Hospitali za umma zinakosa dawa kwa sababu zilichukuliwa na wasimamizi wa hospitali.**
**(Mwanafunzi aongeze hoja zingine zozote.)**


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes